

## Feed the Future Tanzania Inua Vijana

### Muda wa Mradi

Agosti 2017 – Agosti 2022

### Bajeti

Dola za Marekani milioni 19.7

### Maeneo lengwa ya mradi

Iringa, Mbeya, na Zanzibar

### Mtekelezaji

DAI Global LLC.

### Washirika

Pathfinder International

SNV

Khangarue Media

### Mawasiliano ya USAID

Joyce Mndambi

Afisa Mwakilishi wa Mradi

+255 746 700 801

[jmndambi@usaid.gov](mailto:jmndambi@usaid.gov)

### Mawasiliano ya Mtekelezaji

Stephen Terravecchia

Mkuu wa Mradi

+255 769 325 902

[stephen.terravecchia@dai.com](mailto:stephen.terravecchia@dai.com)

### Kwa Mawasiliano Zaidi

Tovuti: [www.usaid.gov/tanzania](http://www.usaid.gov/tanzania)

Facebook: USAIDTanzania

Twitter: @USAIDTanzania



Vijana wa Kitanzania wana uwezo wa kuchangia jukumu muhimu katika maendeleo ya uchumi wa nchi yao, lakini zaidi ya vijana 800,000 wanaoingia katika nguvukazi ya Tanzania kila mwaka, ajira bado ni changamoto. Ili Tanzania ifaidike kwa kuongezeka kwa idadi ya vijana na kufikia malengo ya ajenda yake ya maendeleo, ni muhimu zaidi sasa kuliko hapo awali kuwapa vijana ujuzi, mafunzo, na rasilimali wanazohitaji kuchangia uchumi. Karibu 67% ya nguvukazi nchini Tanzania wanajishughulisha na kilimo. Nchi, inashughulikia ukosefu wa ajira kwa kuhamasisha vijana kuwa na utaalam zaidi katika sekta hiyo. Mradi wa Feed the Future Inua Vijana nchini Tanzania, unaunganisha vijana kupata mafunzo ya ujasiriamali, ujuzi wa kitaalam katika stadi za maisha, uongozi, pamoja na kilimo bora chenye kuzingatia afya, na fursa za ajira. Mradi huu unakusudia kuongeza fursa za mapato kwa vijana 21,500 kupitia mafunzo yakinifu, ya kitaalam na kuwaunganisha vijana kwenye ajira zilizo rasmi na zisizo rasmi.

### MUHTASARI WA MRADI

Utekelezwaji wa mradi wa Feed the Future Inua Vijana unatekelezwa katika mikoa ya Iringa, Mbeya, na Zanzibar, ukishirikiana na serikali za mitaa, sekta binafsi, asasi za kiraia na vijana wenyewe kubadili maoni ya vijana kwa kukuza ujuzi wa kitaalam na uongozi kati ya vijana wenye umri wa miaka 15-35, huku wakikuza mienendo ya kiafya. Mradi unaunganisha vijana na fursa mbali mbali katika malengo yake matatu:

1. Kuongeza ujasiriamali na ujuzi wa utayari wa nguvu kazi na ajira miongoni mwa vijana
2. Kuimarisha uongozi na maendeleo chanya kwa vijana
3. Kuongeza stadi za maisha kwa maisha bora na mipango



Ili kufanikisha malengo haya, mradi wa Feed the Future Tanzania Inua Vijana hutumia njia inayotokana na uhitaji ili kukidhi mahitaji muhimu zaidi katika sekta binafsi, serikali, na wafanyakazi. Kwa kufanya kazi bega kwa bega na biashara za kilimo, na kutambua ujuzi na ustadi unaohitajika kuharakisha ukuaji katika sekta hiyo, programu hii inaunda shughuli zake kulingana na mahitaji na pia hutekeleza kazi zake kwa kutoa ruzuku na kuunganisha vijana na fursa za kujipatia riziki kulingana na maslahi yao, matarajio yao, na uwezo wao.

## MATOKEO

Mkabala mkuu wa mradi wa Feed the Future Tanzania Inua Vijana ni Baraza lake la Kitaifa la Ushauri la Vijana: chombo kinachoongozwa na vijana wenyewe na kufanya kazi zake katika ngazi za wilaya, mkoa na kitaifa, kwa kuhabarisha na kutoa ushauri kwa mradi huo. Baraza hili lilizinduliwa mwaka 2018, kwa kuhakikisha shughuli za mradi zinalenga vijana na kukabiliana na changamoto zinazowakabili vijana katika karne hii vijijini nchini Tanzania.

Takribani katika kukamilisha mwaka wa pili wa utekelezaji wa mradi wa Feed the Future Inua Vijana, mradi umefanikiwa kuwaelimisha vijana zaidi ya 10,000 katika nyanya za ujasiriamali, ujuzi wa utayari wa wafanyakazi, uongozi, na stadi za maisha kwa maisha bora na upangaji. Kupitia katika mafunzo yaliyotolewa iliwezesha uanzishaji na uboreshaji wa biashara ndogo ndogo zinazoongozwa na vijana na uundaji wa ajira zaidi ya 1,000 rasmi na zisizo rasmi. Mafunzo hayo pia yameongeza ushiriki wa vijana katika uongozi wa mitaa, na zaidi ya vijana 300 waliofunzwa wamejiunga na vyombo vya maamuzi na zaidi ya vijana 450 waliofunzwa sasa wanashiriki katika shughuli za maendeleo ya jamii. Kwa kuongezea, zaidi ya vijana 3,600 wamepata huduma za afya ya uzazi wa ujinsia kwa vijana wakati wa rufaa ya shughuli hiyo, na karibu vijana 740 walio katika hatari na mazingira magumu ya kijinsia wamefundishwa juu ya uongozi na stadi za maisha bora. Walakini, kushirikiana na mradi wa Inua Vijana hakuishii na mafunzo tu. Mradi huhimiza washiriki kuendelea kujifunza na kukua na pia kushiriki katika malengo yote matatu: kuwa mhasishaji wa jamii au mwanachama wa Baraza la Vijana au kushiriki katika shughuli za jamii kama mwakilishi wa vijana.

Ili kuongeza upatikanaji wa huduma za kifedha kwa vijana wa vijijini ambao wametengwa, mradi ulifanikiwa kutoa mafunzo na kuhamasisha vijana kuanzisha Mashirika ya Akiba na Mikopo ya Vijana huko Iringa, Mbeya, na Zanzibar. Vikundi 120 vya akiba na mikopo ya vijana vimeanzishwa; na zaidi ya vijana 1,967 wana shiriki katika vikundi hivi, na karibu vijana 1,900 tayari wamechukua mikopo ili kuboresha biashara zao na maisha bora.

